JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS
# TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MWONGOZO WA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI ZA VIJIJI, VITONGOJI NA MITAA UTAKAOFANYIKA TAREHE 27 NOVEMBA, 2024

Umeandaliwa na:
Ofisi ya Rais, TAMISEMI,
Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa TAMISEMI,
S. L. P 1923,
41185 DODOMA.
Simu: (26) 2322607
Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz

**AGOSTI, 2024**

**YALIYOMO**


1.0 UTANGULIZI ........................................................................1

2.0 TANGAZO LA UCHAGUZI..................................................2

3.0 KUTANGAZA MAJINA NA MIPAKA YA VIJIJI, VITONGOJI NA MITAA.................................................... 2

4.0 RATIBA YA SHUGHULI ZA UCHAGUZI .........................3

5.0 KUTOA MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI ................3

6.0 UTEUZI WA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI, WASIMAMIZI WASAIDIZI WA UCHAGUZI NA WASIMAMIZI WA VITUO VYA UCHAGUZI .............. 4

7.0 UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA:...............................5

8.0 SIFA ZA MPIGA KURA........................................................7

9.0 SIFA ZA MGOMBEA.............................................................8

10.0 KUCHUKUA NA KUREJESHA FOMU ZA KUGOMBEA UONGOZI ........................................................................... 9

11.0 SEMINA ZA UCHAGUZI .................................................. 10

12.0 AINA NA IDADI YA WAJUMBE WATAKAOCHAGULIWA................................................. 11

13.0 UDHAMINI WA VYAMA VYA SIASA ............................ 12

14.0 SIKU YA UTEUZI ............................................................... 13

15.0 UTARATIBU WA UTEUZI WA MGOMBEA PEKEE13

16.0 PINGAMIZI KUHUSU UTEUZI....................................... 13

17.0 KAMATI YA RUFANI .................................................................... 14
18.0 KAMPENI ZA UCHAGUZI................................................. 15
19.0 UTARATIBU WA KUPIGA KURA....................................... 16
20.0 UTARATIBU WA UPIGAJI KURA KWA MGOMBEA PEKEE ................................................................................... 20
21.0 KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI ............................................................................20
22.0 VIFAA VITAKAVYOTUMIKA KWENYE UCHAGUZI: ....................................................................................................22
23.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA TAARIFA NA MATOKEO YA UCHAGUZI ...............................................23
24.0 UTARATIBU WA UTUNZAJI NA UTEKETEZAJI WA NYARAKA ZA UCHAGUZI ................................................. 24
25.0 USHIRIKI WA VYAMA VYA SIASA................................ 24
26.0 NAFASI WAZI........................................................................ 25
27.0 ELIMU YA MPIGA KURA.................................................... 27
28.0 M W I S H O ........................................................................... 28

# MWONGOZO WA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA NGAZI ZA VIJIJI, VITONGOJI NA MITAA UTAKAOFANYIKA TAREHE 27 NOVEMBA, 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu wa Uchaguzi wa viongozi wa Vitongoji, Vijiji na Mitaa umeandaliwa kwa lengo la kufafanua kwa lugha rahisi maudhui ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi za msingi. Kwa mujibu wa mwongozo huu ngazi za msingi za Serikali za mitaa zina maana ya Mitaa katika Mamlaka za Miji, Vijiji na Vitongoji katika Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji zenye Vijiji na Vitongoji.

Kwa kufafanua kwa lugha rahisi mwongozo huu utawasaidia, Wasimamizi, Wasimamizi Wasaidizi, Wasimamizi wa Vituo vya Uchaguzi na Wadau wengine wa Uchaguzi kufahamu majukumu yao katika kusimamia mchakato mzima wa Uchaguzi. Aidha, Mwongozo huu utawawezesha wadau wa Uchaguzi, pamoja na mambo mengine, kufahamu haki na wajibu wa vyama vya siasa na wapiga kura.

Ni mategemeo ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kuwa, kupitia Mwongozo huu, Uchaguzi utafanyika katika mazingira huru, uwazi, amani na haki kwa washiriki wote. OR – TAMISEMI kama Mamlaka ya Uchaguzi inatarajia kuwa Wasimamizi, Wasimamizi Wasaidizi, Wasimamizi wa Vituo, Mawakala na Wadau wengine wote wa Uchaguzi watashiriki katika shughuli za Uchaguzi wakizingatia maslahi mapana ya nchi yetu ikiwa ni pamoja na kudumisha demokrasia na kuimarisha amani, utulivu, mshikamano na umoja wa kitaifa.

Pamoja na kufafanua Kanuni za Uchaguzi kwa lugha rahisi, Mwongozo huu umejumuisha pia mtiririko wa matukio ya

Uchaguzi kuanzia tarehe ya Tangazo la Uchaguzi hadi tarehe ya Uchaguzi. Ratiba ya Uchaguzi imefanywa kuwa ni sehemu ya Mwongozo huu ili kurahisisha rejea.

## 2.0 TANGAZO LA UCHAGUZI

**2.1** Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambaye ndiye mwenye dhamana ya Uchaguzi atatakiwa kutoa Tangazo la Uchaguzi tarehe 15 Agosti, 2024 litakaloainisha ratiba ya uchaguzi, shughuli zinazohusiana na uchaguzi na masharti muhimu ya Uchaguzi.

**2.2** Tangazo hilo litatolewa katika Magazeti ya Kiswahili na Kiingereza yanayosambazwa nchi nzima na katika vyombo vingine vya habari.

**2.3** Kutolewa kwa Tangazo kutakuwa ni mwanzo wa mchakato mzima wa shughuli za Uchaguzi.

## 3.0 KUTANGAZA MAJINA NA MIPAKA YA VIJIJI, VITONGOJI NA MITAA

**3.1** Kila Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kubandika katika sehemu ya matangazo ya uchaguzi majina ya maeneo na mipaka ya kila mtaa, kitongoji au kijiji kwa wakazi wa maeneo hayo kwa kuzingatia orodha ya vijiji, vitongoji na mitaa iliyotangazwa katika Gazeti la Serikali.

**3.2** Tangazo la majina na mipaka ya vijiji, vitongoji na mitaa litabandikwa tarehe 16 Septemba, 2024.

**3.3** Utaratibu huu una lengo la kuwawezesha wakazi kutambua na kufahamu mipaka ya maeneo ya Uchaguzi.

## 4.0 RATIBA YA SHUGHULI ZA UCHAGUZI

**4.1** Kila Msimamizi wa Uchaguzi na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atatakiwa kuzingatia ratiba ya matukio ya Uchaguzi kama ilivyo katika Kanuni za Uchaguzi na kama ambavyo yatakuwa yamefafanuliwa katika Mwongozo huu.

**4.2** Kila Msimamizi wa Uchaguzi atahakikisha anatoa elimu kwa umma na wadau mbalimbali kuhusu Uchaguzi katika Halmashauri husika.

**4.3** Kila Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kufahamu idadi ya vijiji, vitongoji au mitaa itakayohusika kufanya Uchaguzi na kufahamu idadi ya wakazi waliojiandikisha kupiga kura ili kuandaa na kupeleka idadi ya kutosha ya vifaa vya uchaguzi wakati wa upigaji kura katika kila eneo.

## 5.0 KUTOA MAELEKEZO KUHUSU UCHAGUZI

**5.1** Wasimamizi wa Uchaguzi watatoa maelekezo kuhusu Uchaguzi tarehe 26 Septemba, 2024.

**5.2** Maelekezo hayo yataelezea masuala muhimu yafuatayo:

(a) tarehe ya kufanyika kwa Uchaguzi ambayo ni tarehe 27 Novemba, 2024;

(b) muda na sehemu ya kuandikisha wapiga kura;

(c) mahali na muda utakapofanyika uchaguzi;

(d) kuwataka wakazi wote wenye sifa za kupiga kura kujiandikisha ili washiriki uchaguzi;

(e) kuwataka wakazi wenye umri wa miaka ishirini na moja au zaidi wanaotaka kugombea nafasi ya uenyekiti wa kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji, au uenyekiti wa kitongoji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa kamati ya mtaa kuchukua fomu za kugombea zinazopatikana kwenye Ofisi ya Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi;

(f) tarehe, muda na mahali pa kuchukua na kurudisha fomu. Muda huo hautazidi siku saba, yaani kuanzia tarehe 01 Novemba hadi tarehe 7 Novemba, 2024;

(g) siku ya uteuzi wa wagombea wa Uchaguzi ambayo itakuwa tarehe 8 Novemba, 2024;

(h) muda wa kuwasilisha pingamizi dhidi ya uteuzi wa mgombea yeyote ambao utaanza tarehe 8, Novemba hadi tarehe 9 Novemba, 2024;

(i) kipindi cha kuendesha mikutano ya kampeni za Uchaguzi ambacho kitakuwa ni siku saba kabla ya siku ya Uchaguzi kuanzia tarehe 20 Novemba hadi tarehe 26 Novemba, 2024; na

(j) masuala mengine yanayohusu Uchaguzi.

## 6.0 UTEUZI WA MSIMAMIZI WA UCHAGUZI, WASIMAMIZI WASAIDIZI WA UCHAGUZI NA WASIMAMIZI WA VITUO VYA UCHAGUZI

**6.1** kutakuwa na Msimamizi wa Uchaguzi, atakayeteuliwa kusimamia uchaguzi;

**6.2** kutakuwa na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo vya Uchaguzi kwa kila mtaa,

kitongoji na kijiji watakaoteuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi;

**6.3** Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo vya Uchaguzi watakaoteuliwa wanatakiwa kuwa na sifa zifuatazo: -

(a) Wasiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa;

(b) Wawe ni watumishi katika Utumishi wa Umma;

(c) Wawe waadilifu.

**6.4** Uteuzi wa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo vya Uchaguzi utafanyika kuanzia tarehe 19 Septemba hadi tarehe 25 Septemba 2024.

## 7.0 UANDIKISHAJI WA WAPIGA KURA: -

**7.1** Msimamizi wa Uchaguzi atateua Mtumishi wa Umma mwenye sifa na uadilifu ambaye ataandikisha na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura.

**7.2** Uteuzi wa Watumishi wa Umma watakaoandikisha wapiga kura na kuandaa Orodha ya Wapiga Kura utafanyika tarehe 6 Oktoba, 2024.

**7.3** Uandikishaji utafanyika katika kitongoji kwa ajili ya uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji. Aidha, kwa upande wa mitaa uandikishaji utafanyika katika mtaa kwa ajili ya uchaguzi wa mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa.

**7.4** Uandikishaji wa wapiga kura utafanyika kwa muda wa siku kumi kuanzia tarehe 11 Oktoba, 2024 hadi tarehe 20 Oktoba 2024.

**7.5** Uandikishaji wa wapiga kura utafanyika kwenye majengo ya umma na pale ambapo hakuna jengo la umma, uandikishaji utafanyika sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atakuwa amekubaliana na viongozi wa vyama vya siasa.

**7.6** Majengo ya vyombo vya usalama, taasisi za dini na vyama vya siasa hayatatumika katika zoezi la uandikishaji wa wapiga kura.

**7.7** Vituo vya uandikishaji wa wapiga kura vitafunguliwa saa mbili kamili asubuhi na kufungwa saa kumi na mbili kamili jioni.

**7.8** Vyama vya Siasa vitaruhusiwa kuweka mawakala wao wakati wa uandikishaji wa wapiga kura kwa gharama zao.

**7.9** Wakati wa uandikishaji wananchi hawataulizwa masuala yanayohusu shughuli zao, uanachama wa chama cha siasa au dini.

**7.10** Tarehe 21 Oktoba, 2024 Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atabandika nakala ya orodha ya wapiga kura katika sehemu ya matangazo ya Uchaguzi kuwezesha wananchi wakague orodha ya wapiga Kura ili:

(a) kuweka pingamizi kuhusu usahihi wa orodha hiyo;

(b) kuomba orodha irekebishwe ili-

i. kurekebisha jina lake;

ii. kubadilisha taarifa zilizopo katika orodha hiyo; au

iii. Kufuta jina lililoorodheshwa kwa vile aliyeorodheshwa amefariki au amekosa sifa za mpiga kura.

**7.11** Mkazi aliyejiandikisha kupiga kura atakuwa na haki ya kuweka pingamizi katika muda wa siku saba kuanzia tarehe 21 Oktoba, 2024 hadi tarehe 27 Oktoba,2024.

**7.12** Pingamizi dhidi ya mtu kuandikishwa kuwa mpiga kura litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atatakiwa kulitolea uamuzi ndani ya muda wa siku mbili tangu tarehe ya mwisho ya ukaguzi wa Orodha ya Wapiga kura yaani tarehe 27 Oktoba hadi tarehe 28 Oktoba, 2024.

## 8.0 SIFA ZA MPIGA KURA

**8.1** Mpiga Kura atatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) ana umri wa miaka 18 au zaidi;

(c) ni mkazi wa kijiji au kitongoji au mtaa ambao Uchaguzi unafanyika;

(d) ana akili timamu; na

(e) awe amejiandikisha kupiga kura katika kitongoji au mtaa au kijiji husika.

**8.2** Mpiga kura atapoteza sifa ya kupiga kura endapo:

(a) hana moja wapo ya sifa zilizoainishwa katika aya ya 8.1;

(b) amejiandikisha kupiga kura katika kituo zaidi ya kimoja.

## 9.0 SIFA ZA MGOMBEA

**9.1** Mkazi yeyote wa kijiji au kitongoji au mtaa anaweza kugombea nafasi yoyote katika Uchaguzi endapo:

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) ana umri wa miaka 21 au zaidi;

(c) anaweza kusoma na kuandika Kiswahili au Kiingereza;

(d) ana shughuli halali ya kumwezesha kuendesha maisha;

(e) ni mwanachama wa chama cha siasa na amedhaminiwa na chama hicho; na

(f) ana akili timamu.

**9.2** Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi yoyote katika uchaguzi endapo:

(a) amepoteza sifa zilizoainishwa katika aya ya 9.1;

(b) amehukumiwa hukumu ya kifo na Mahakama za Tanzania au anatumikia kifungo cha zaidi ya miezi sita gerezani;

(c) hajatangaza kuwepo kwa mkataba au maslahi katika kampuni yenye mkataba na kijiji ambacho anataka kugombea;

(d) amepoteza sifa ya kupiga kura; au

(e) ataajiriwa au kuteuliwa katika wadhifa wowote katika Utumishi wa Umma au kuchaguliwa katika nafasi ya udiwani, ubunge, uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, umakamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

## 10.0 KUCHUKUA NA KUREJESHA FOMU ZA KUGOMBEA UONGOZI

**10.1** Wasimamizi wa Uchaguzi wataandaa fomu za uteuzi wa kugombea nafasi zilizotajwa katika Kanuni na Mwongozo huu. Kila fomu itakuwa na nembo ya Halmashauri.

**10.2** Fomu za kugombea nafasi za uongozi katika uchaguzi zitatolewa kuanzia tarehe 01 Novemba hadi tarehe 7 Novemba 2024, kuanzia saa moja na nusu asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

**10.3** Fomu itakayorudishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi bila kujazwa kwa kuzingatia matakwa ya kanuni haitatambuliwa na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi katika kufanya uteuzi;

**10.4** Kila Msimamizi wa Uchaguzi atatakiwa kuhakikisha kuwa fomu za uteuzi wa wagombea zinakuwepo za kutosha na zitatolewa bila masharti wala malipo ya aina yoyote.

**10.5** Mtu aliyechukua fomu ya kugombea nafasi ya uongozi atahakikisha anarejesha fomu husika ndani ya muda wa siku saba tangu siku ya kwanza ya utoaji wa fomu na baada ya fomu kurejeshwa mwombaji atapewa nakala moja na nakala moja itabaki kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi.

**10.6** Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi hatoruhusiwa kupokea kutoka kwa mtu yeyote fomu za uteuzi zitakazowasilishwa baada ya saa kumi kamili jioni ya siku ya mwisho ya kurejesha fomu.

## 11.0 SEMINA ZA UCHAGUZI

**11.1** Wasimamizi wa Uchaguzi watatakiwa kufanya maandalizi ya kutosha na kuandaa semina ambazo Kanuni za Uchaguzi zitajadiliwa na kueleweka kwa Wasimamizi Wasaidizi na maafisa watakaohusika katika ngazi zote pamoja na viongozi wa vyama vya siasa.

**11.2** Wasimamizi wa Uchaguzi kwa kushirikiana na/au kwa kuwatumia Watumishi wa Umma watakuwa wakufunzi wa Semina za uchaguzi katika maeneo yao.

**11.3** Semina hizi zitafanyika kwa kupitia na kusoma mwongozo huu wa uchaguzi, ratiba yake; kanuni za uchaguzi kuanzia za mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya kijiji; mwenyekiti wa kitongoji, mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa.

Msisitizo utolewe kuhusu hatua zote muhimu za uchaguzi, muda, na fomu za uchaguzi ili kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru na wa haki.

## 12.0 AINA NA IDADI YA WAJUMBE WATAKAOCHAGULIWA

**12.1** Halmashauri ya Kijiji itakuwa na wajumbe wasiozidi ishirini na tano watakaochaguliwa na wakazi wa vitongoji katika kijiji kama ifuatavyo:

(a) Mwenyekiti wa Kijiji;

(b) Wenyeviti wa vitongoji vilivyomo katika eneo la kijiji;

(c) Wajumbe mchanganyiko wanawake na wanaume; na

(d) Wajumbe wa kundi la wanawake ambao idadi yao haitakuwa chini ya theluthi moja ya wajumbe wote wa Halmashauri ya kijiji.

**12.2** Kamati ya Mtaa itakuwa na wajumbe wasiozidi sita watakaochaguliwa na wakazi wa mtaa. Wajumbe hao ni wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Mtaa;

(b) Wajumbe wengine watano ambao kati yao wajumbe wasiopungua wawili watakuwa wanawake.

**12.3** Wenyeviti wa vitongoji watakaochaguliwa kutoka kila kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo.

## 13.0 UDHAMINI WA VYAMA VYA SIASA

**13.1** Wagombea wa nafasi zote za uongozi watatakiwa kudhaminiwa na vyama vyao vya siasa.

**13.2** Kwa kuzingatia kwamba kila chama kina utaratibu wake wa kuteua au kutoa udhamini kwa wagombea wake, Wasimamizi wa Uchaguzi watatoa maelekezo mapema kwa Wasimamizi Wasaidizi kuzingatia yafuatayo wakati fomu zitakaporejeshwa:

(a) Mgombea atahesabiwa kuwa amepata udhamini wa chama chake cha siasa endapo fomu ya maombi ya kugombea itakuwa imeidhinishwa na ngazi ya chini kabisa katika muundo wa chama chake;

(b) Kwa nafasi ya uenyekiti kila chama cha siasa kitatakiwa kutoa mgombea mmoja. Endapo kutatokea wagombea zaidi ya mmoja kutoka chama kimoja cha siasa kwa nafasi hiyo, basi yule aliyeteuliwa na ngazi ya chini kabisa ndiye atahesabika kuwa mgombea mwenye udhamini halali;

(c) Kwa nafasi za ujumbe wa Halmashauri ya kijiji au Kamati ya Mtaa hakutakuwa na ukomo wa idadi ya wagombea kwa chama cha siasa. Chama cha siasa kinaweza kusimamisha wagombea wa nafasi hizo kulingana na nafasi zote zinazogombewa;

(d) Kiongozi au afisa wa chama cha siasa ambaye atathibitisha udhamini katika fomu ya mgombea atatakiwa:

(i) kuandika majina yake matatu;

(ii) kutaja wadhifa wake katika chama; na

(iii) kugonga mhuri wa chama.

(e) Mgombea atatakiwa kujaza nakala mbili (2) kwa kila ombi na zote zitatakiwa kuwa na saini ya kiongozi wa chama cha siasa na mhuri wa chama cha mgombea ikiwa ni uthibitisho wa kudhaminiwa kwake;

(f) Mwisho wa kurudisha fomu ya kugombea utakuwa saa kumi kamili jioni ya tarehe 7 Novemba, 2024.

## 14.0 SIKU YA UTEUZI

Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atafanya uteuzi wa wagombea wa nafasi za uongozi katika ngazi zote tarehe 8 Novemba, 2024.

## 15.0 UTARATIBU WA UTEUZI WA MGOMBEA PEKEE

Endapo kutakuwa na mgombea mmoja halali wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji, kitongoji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa kamati ya mtaa Msimamizi Msaidizi wa uchaguzi atamteua mwombaji huyo kuwa mgombea pekee kwa nafasi aliyoomba.

## 16.0 PINGAMIZI KUHUSU UTEUZI

**16.1** Mgombea au mtu aliyeomba kuteuliwa anaweza kuweka pingamizi kuhusu uteuzi wa wagombea.

**16.2** Pingamizi dhidi ya uteuzi wa wagombea litawasilishwa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuanzia tarehe 8 Novemba hadi tarehe 9 Novemba, 2024 na Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atasikiliza na kutoa uamuzi kuanzia tarehe 8 Novemba hadi tarehe 10 Novemba, 2024.

## 17.0 KAMATI YA RUFANI

**17.1** Makatibu Tawala wa Mikoa watateua wajumbe wa Kamati za Rufani kwa kila Wilaya ambao watasikiliza na kuamua pingamizi linalohusu uteuzi wa wagombea katika Wilaya husika tarehe 01 Novemba, 2024. Uteuzi utazingatia jinsia.

**17.2** Wajumbe wa Kamati ya Rufani ni wafuatao:-

(a) Katibu Tawala wa Wilaya ambaye atakuwa Mwenyekiti;

(b) Watumishi wa Umma wanne kutoka katika Taasisi za Umma zilizopo katika Wilaya husika; na

(c) Mtumishi mmoja wa Umma kutoka Ofisi ya KatibuTawala wa Wilaya ambaye atakuwa Katibu.

**17.3** Watu wafuatao hawataruhusiwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Rufani:

(a) Watu wanaohusika na uteuzi wa wagombea kama vile Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi na Msimamizi wa Kituo;

(b) Watumishi wa Halmashauri;

(c) Watumishi katika vyombo vya ulinzi na usalama; na

(d) Viongozi wa Vyama vya Siasa katika ngazi yoyote.

**17.4** Mgombea au mtu ambaye aliomba kugombea ambaye hataridhika na uamuzi wa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi kuhusu uteuzi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye Kamati ya Rufani kuanzia tarehe 10 Novemba hadi tarehe 13 Novemba, 2024. Muda wa kushughulikia rufaa utakuwa ni kuanzia tarehe 10 Novemba hadi tarehe 13 Novemba, 2024.

**17.5** Uamuzi wa Kamati ya Rufani kuhusu rufaa dhidi ya pingamizi la uteuzi utakuwa wa mwisho.

## 18.0 KAMPENI ZA UCHAGUZI:

**18.1** Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 20 Novemba hadi tarehe 26 Novemba, 2024.

**18.2** Wagombea kwenye ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa au wawakilishi wao au vyama vya siasa wanaweza kuitisha mikutano ya kampeni kwa kufuata ratiba itakayowasilishwa na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa na kuratibiwa na Msimamizi wa Uchaguzi.

**18.3** Vyama vya Siasa vyenye wagombea vinaweza kuwateua wanachama wake kuendesha kampeni kwa niaba ya wagombea w a vyama vyao.

**18.4** Kampeni za uchaguzi zitaanza saa mbili asubuhi na zitamalizika saa kumi na mbili jioni ya kila siku ya kampeni.

**18.5** Vyombo vya ulinzi na usalama hususan Jeshi la Polisi, Jeshi la akiba (Mgambo) wenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi, vitatumika katika kuhakikisha kunakuwepo na usalama na utulivu katika mikutano ya kampeni na wakati wa uchaguzi. Vikundi vya ulinzi vya jadi au binafsi au vya mashabiki wa vyama vya siasa havitaruhusiwa kutumika kwenye maeneo ya mikutano ya kampeni au ya uchaguzi.

**18.6** Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watatakiwa kuhakikisha vikundi vya uhamasishaji vya vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi vinatumika kwa madhumuni ya uhamasishaji na si vinginevyo.

## 19.0 UTARATIBU WA KUPIGA KURA

**19.1** Uchaguzi utafanyika tarehe 27 Novemba, 2024 kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni.

**19.2** Uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, mwenyekiti wa kitongoji na wajumbe wa Halmashauri ya kijiji utafanyika katika vitongoji vilivyomo katika vijiji kwa Mamlaka za Wilaya na Mamlaka za Miji zenye Vijiji.

**19.3** Uchaguzi wa mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa utafanyika katika mitaa iliyomo katika Mamlaka za Miji.

**19.4** Uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika Mamlaka za Miji Midogo utafanyika katika vitongoji vilivyoko katika Mamlaka hizo.

**19.5** Kabla ya kuanza kupiga kura, Msimamizi wa Kituo atawaonesha wapiga kura sanduku la kupigia

kura lililo wazi na atalifunga kwa lakiri kwa namna ambayo itazuia kufunguliwa bila kukata lakiri.

**19.6** Kabla ya Msimamizi wa Kituo hajampatia mpiga kura karatasi za kupigia kura, atajiridhisha kama jina la mpiga kura limeorodheshwa katika orodha ya wapiga kura.

**19.7** Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura aoneshe kitambulisho kitakachoonesha kuwa jina la mpiga kura huyo ndilo lililomo kwenye orodha ya wapiga kura. Aina ya kitambulisho ambacho Msimamizi wa Kituo anaweza kumtaka mpiga kura kuonesha ni pamoja na:

(a) kitambulisho cha mpiga kura;

(b) kitambulisho cha kazi;

(c) hati ya kusafiria;

(d) kadi ya bima ya afya;

(e) kitambulisho cha shule au chuo;

(f) kitambulisho cha mifuko ya hifadhi ya jamii;

(g) leseni ya udereva; au

(h) kitambulisho cha taifa.

**19.8** Endapo mpiga kura atakuwa hana kitambulisho cha aina yoyote kilichotajwa katika kanuni za uchaguzi, lakini jina lake limo kwenye orodha ya wapiga kura iliyoandaliwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi atamruhusu mtu

huyo kupiga kura baada ya kutambuliwa na wakazi wa eneo husika.

**19.9** Kwenye ngazi ya Mtaa: -

Kwa kuzingatia kuwa wajumbe wa Kamati ya Mtaa ni sita, wawili miongoni mwao wakiwa ni wanawake, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi tatu za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo: -

(a) nafasi moja ya Mwenyekiti;

(b) nafasi tatu za wajumbe wa Kamati ya Mtaa kutoka kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake; na

(c) nafasi mbili za wajumbe wa Kamati ya Mtaa kutoka kundi la wanawake.

**19.10** Kwenye ngazi ya vitongoji vilivyoko katika Mamlaka za Miji Midogo, uchaguzi utakuwa ni wa mwenyekiti wa kitongoji tu. Hivyo, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi moja ya kupigia kura kwa ajili ya kuchagua mwenyekiti wa kitongoji.

**19.11** Kwenye ngazi ya Kijiji:-

Kwa kuzingatia kuwa idadi ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji haitazidi wajumbe ishirini na tano, theluthi moja miongoni mwao wakiwa ni wanawake, Msimamizi wa Kituo atampatia mpiga kura karatasi nne za kupigia kura kwa nafasi zifuatazo: -

(a) Mwenyekiti wa Kijiji;

(b) Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji wa kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake;

(c) Wajumbe wa kundi la wanawake; na

(d) Mwenyekiti wa Kitongoji.

**19.12** Kura zitakuwa za siri na zitapigwa katika majengo ya umma au sehemu ambayo Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ataiteua baada ya kushauriana na wagombea, wawakilishi wao au vyama vya siasa.

**19.13** Majengo ya vyombo vya usalama, taasisi za dini na vyama vya siasa hayatatumika katika zoezi la kupiga kura.

**19.14** Mpiga kura ambaye ana mahitaji maalumu anaweza kumwomba mtu yeyote aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, mgombea au mwakilishi wake.

**19.15** Mpiga kura ambaye hajui kusoma na kuandika anaweza kumwomba mtu yeyote aliyemchagua yeye mwenyewe kumsaidia kupiga kura isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Msimamizi wa Kituo, Mgombea au Mwakilishi wake.

**19.16** Mtu mmoja hatoruhusiwa kumsaidia mpiga kura zaidi ya mmoja.

## 20.0 UTARATIBU WA UPIGAJI KURA KWA MGOMBEA PEKEE

Mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa kijiji, kitongoji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa kamati ya mtaa, aliyetangazwa kuwa mgombea pekee atapigiwa kura ya NDIYO au HAPANA.

## 21.0 KUHESABU KURA NA KUTANGAZA MATOKEO YA UCHAGUZI

**21.1** Msimamizi wa Kituo atahesabu kura mbele ya wagombea, mawakala, Msimamizi wa Uchaguzi, Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi, Askari polisi au Askari wa jeshi la akiba(mgambo) mwenye sare au Afisa yeyote anayesimamia ulinzi na mwangalizi wa uchaguzi mwenye kitambulisho kwenye kituo cha kupigia kura. Kabla ya kuanza kuhesabu kura, Msimamizi wa Kituo atafanya yafuatayo:

(i) atahakiki idadi ya wakazi waliopiga kura;

(ii) atahesabu idadi ya karatasi za kupigia kura ambazo hazikutumika na kuziweka katika bahasha maalum;

(iii) atakagua lakiri na kuona kama haijafunguliwa;

(iv) atakata lakiri; na

(v) atafungua sanduku la kupigia kura.

**21.2** Baada ya zoezi la kuhesabu kura kukamilika, Msimamizi wa Kituo atamtangaza mgombea wa nafasi ya uenyekiti wa kitongoji, kijiji au mtaa, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji au ujumbe wa

Kamati ya Mtaa aliyepata kura nyingi kuwa mshindi.

**21.3** Endapo idadi ya kura kwa nafasi ya uenyekiti wa kijiji au mtaa zitalingana kwa wagombea wanaoongoza kura, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

**21.4** Endapo idadi ya kura kwa nafasi ya uenyekiti wa kitongoji zitalingana kwa wagombea wanaoongoza kura, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atawasilisha taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apange tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

**21.5** Mgombea pekee kwa nafasi ya uenyekiti wa kitongoji, kijiji au mtaa atakuwa amechaguliwa endapo atapata kura nyingi za NDIYO kati ya kura zote halali zilizopigwa.

**21.6** Endapo mgombea pekee kwa nafasi ya uenyekiti wa kijiji au mtaa atashindwa kupata kura nyingi za NDIYO au idadi ya kura za NDIYO au HAPANA zitalingana, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Msimamizi wa Uchaguzi ambaye atapanga tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi.

**21.7** Endapo mgombea pekee kwa nafasi ya uenyekiti wa kitongoji, atashindwa kupata kura nyingi za NDIYO

au idadi ya kura za NDIYO au HAPANA zitalingana, Msimamizi wa Kituo atatangaza matokeo hayo na kuwasilisha taarifa hiyo kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ambaye atawasilisha taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi ili apange tarehe nyingine ya uchaguzi ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya uchaguzi**.**

## 22.0 VIFAA VITAKAVYOTUMIKA KWENYE UCHAGUZI:

Vifaa vifuatavyo vitatumika katika uchaguzi:-

(a) Orodha ya wapiga kura wenye sifa za kupiga kura kwa eneo husika;

(b) karatasi za kupiga kura;

(c) meza moja ambayo itatumika wakati wa kuhesabu kura;

(d) masanduku ya kupigia kura yenye kuonesha kitu kilichomo ndani ya sanduku;

(e) mifuko mikubwa ya kawaida itakayotunza kura baadaa kuhesabiwa na uchaguzi kukamilika;

(f) Fomu za matokeo ya uchaguzi;

(g) Fomu za kuomba kugombea; na

(h) Mihuri ya Halmashauri ya Kijiji au Serikali ya Kijiji kwa maeneo ya vijiji na vitongoji; na mhuri wa Mtendaji wa Mtaa au Kata kwa uchaguzi wa viongozi wa mitaa.

## 23.0 UTARATIBU WA KUWASILISHA TAARIFA NA MATOKEO YA UCHAGUZI

**23.1** Matokeo ya uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji, wenyeviti wa vitongoji na mitaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa yatajazwa kwenye Fomu maalum ambayo itasainiwa na wagombea au wawakilishi wao pamoja na Msimamizi wa Kituo na kubandikwa kwenye sehemu ya matangazo ya uchaguzi.

**23.2** Nakala za matokeo ya uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji na wwa Halmashauri ya vijiji kutoka katika vitongoji zitawasilishwa Ofisi ya Serikali ya Kijiji kwa ajili ya kujumlishwa na kutangazwa washindi.

**23.3** Matokeo ya uchaguzi wa mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa yatatangazwa katika ngazi ya mtaa husika.

**23.4** Matokeo ya mwenyekiti wa kitongoji yatatangazwa katika ngazi ya kitongoji husika.

**23.5** Wasimamizi wa vituo vya uchaguzi watatakiwa kuwasilisha matokeo ya uchaguzi kupitia fomu maalum zilizoainishwa kwenye kanuni za uchaguzi kwa Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya mtaa au kijiji yenye taarifa zifuatazo:

(a) majina ya wagombea, vyama vyao vya siasa na idadi ya kura walizopata;

(b) idadi ya wakazi waliojiandikisha;

(c) idadi ya wakazi waliopiga kura; na

(d) idadi ya kura zilizoharibika au kukataliwa.

**23.6** Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi ngazi ya mtaa na kijiji wataunganisha taarifa zinazotoka kwenye vitongoji na mitaa na kuziwasilisha kwa Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya kata ambaye naye ataziwasilisha kwa Msimamizi wa Uchaguzi.

**23.7** Msimamizi wa Uchaguzi ataunganisha taarifa zote za matokeo ya uchaguzi na kuweka kumbukumbu zake na kisha kutuma taarifa ya matokeo ya uchaguzi yenye kuonyesha taarifa zilizoelezwa katika aya ya 23.5 kwa Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na nakala kwa Katibu Tawala wa Mkoa.

## 24.0 UTARATIBU WA UTUNZAJI NA UTEKETEZAJI WA NYARAKA ZA UCHAGUZI

Msimamizi wa Uchaguzi atahakikisha anatunza kwa usalama nyaraka zote zinazohusu uendeshaji wa uchaguzi. Baada ya siku thelathini tangu kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi, Msimamizi wa Uchaguzi atateketeza karatasi za kupigia kura na fomu za uteuzi za wagombea zilizotumika isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo kwa amri ya Mahakama kutokana na mwenendo wa mashauri ya uchaguzi.

## 25.0 USHIRIKI WA VYAMA VYA SIASA

**25.1** Wasimamizi wa Uchaguzi watatakiwa kuitisha mkutano wa siku moja wa baina yao na viongozi wa vyama vya siasa ngazi ya Wilaya vyenye usajili wa kudumu ili:-

(a) kutoa elimu juu ya uchaguzi wa viongozi wa ngazi za vijiji, vitongoji na mitaa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi;

(b) kuelekeza utaratibu utakaotumika kuandikisha wapiga kura kwenye orodha ya piga kura;

(c) kuelezea sifa za wapiga kura na sifa za wagombea;

(d) kuweka bayana idadi ya vijiji, vitongoji na mitaa iliyopo kwenye eneo la Halmashauri; na

(e) kuelezea ratiba ya matukio yote muhimu hadi siku ya uchaguzi.

**25.2** Kila chama cha siasa kitawajibika kugharamia ushiriki wa wajumbe wake katika mkutano huo.

## 26.0 NAFASI WAZI

**26.1** Nafasi ya uenyekiti wa kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya kijiji, uenyekiti wa kitongoji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itakuwa wazi endapo yatatokea mambo yafuatayo:

(a) kifo cha mwenyekiti au mjumbe;

(b) Mwenyekiti au Mjumbe kujiuzulu wadhifa wake;

(c) Mwenyekiti au mjumbe kukosa sifa za kuwa mgombea;

(d) kubatilishwa kwa matokeo ya uchaguzi;

(e) Mwenyekiti au mjumbe kukoma kuwa mwanachama wa chama cha siasa kilichomdhamini;

(f) Mwenyekiti au mjumbe kuhama kijiji, kitongoji au mtaa kwa kadri itakavyokuwa;

(g) Mwenyekiti kutoitisha mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu za msingi;

(h) Mwenyekiti au mjumbe kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya kawaida bila kuwa na sababu ya msingi;

(i) kugawanywa kwa kijiji, kitongoji au mtaa; au

(j) Mwenyekiti au mjumbe kuvuliwa madaraka kwa mujibu wa Sheria.

**26.2** Endapo litatokea jambo lolote litakalo sababisha nafasi wazi ya uongozi, Mtendaji wa Kijiji au Mtaa atatoa taarifa kwa Msimamizi wa Uchaguzi katika kipindi kisichozidi siku saba tangu kutokea kwa jambo hilo.

**26.3** Msimamizi wa Uchaguzi atatangaza kuwepo kwa nafasi wazi ya uenyekiti wa kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji, uenyekiti wa kitongoji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji au Mtaa juu ya kuwepo kwa nafasi wazi.

**26.4** Nafasi ya uenyekiti wa kijiji, ujumbe wa Halmashauri ya Kijiji, uenyekiti wa kitongoji, uenyekiti wa mtaa au ujumbe wa Kamati ya Mtaa itajazwa katika muda wa siku sitini baada ya kutangazwa kuwa wazi.

## 27.0 ELIMU YA MPIGA KURA

**27.1** Mara baada ya tangazo la uchaguzi kutolewa, taasisi yoyote inayokusudia kutoa elimu ya mpiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa, inaweza kuwasilisha maombi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Maombi hayo yataambatishwa na nyaraka zifuatazo:

(i) Cheti cha usajili;

(ii) barua ya usajili kuthibitisha uhai wa taasisi;

(iii) Katiba ya taasisi;

(iv) majina na anwani za viongozi wa taasisi;

(v) namba za simu za taasisi au viongozi;

(vi) Anwani ya ofisi;

(vii) Taarifa ya fedha inayoonesha vyanzo vya fedha;

(viii) Taarifa ya rasilimali watu na vitendea kazi katia utoaji elimu; na

(ix) Vibali vya kazi kwa wasio raia wa Tanzania.

**27.2** Taasisi ambazo zitapewa kibali cha kutoa elimu ya mpiga kura, zitatoa elimu ya mpiga kura kwa gharama zao wenyewe.

## 28.0 M W I S H O

Mwongozo huu wa uchaguzi ni rejea rahisi ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2024 na siyo mbadala wa Kanuni za uchaguzi. Endapo kutatokea kukinzana kati ya Kanuni na mwongozo, Kanuni za uchaguzi ndizo zitakazo kuwa na nguvu.

Wasimamizi wa Uchaguzi, Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi, Wasimamizi wa Vituo na wadau wote katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa watakaohusika na shughuli za Uchaguzi wanatakiwa kusoma na kuzingatia kwa makini Kanuni za Uchaguzi pamoja na miongozo mbalimbali ambayo Waziri Mwenye dhamana anaweza kutoa atakapoona inafaa.

..............................................

DODOMA
15 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa*

## JEDWALI LA MATUKIO YA UCHAGUZI

| Na. | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 1. | Tangazo la Uchaguzi kwa Umma | 15 Agosti, 2024 | Waziri Nchi, OR-TAMISEMI |
| 2. | Maombi ya kuangalia uchaguzi | 30 Agosti-17 Septemba, 2024 | Katibu Mkuu , OR-TAMISEMI |
| 3. | Tangazo la majina na mipaka ya Vijiji na Vitongoji | 16 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 4. | Uteuzi wa Wasimamizi wasaidizi wa Uchaguzi na Wasimamizi wa Vituo. | 19-25 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 5. | Maelezo kuhusu Uchaguzi | 26 Septemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 6. | Semina kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi na wasimamizi wa vituo | 30 Septemba,2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 7. | Uteuzi wa waandikishaji wa wapiga kura. | 6 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Uchaguzi |
| 8. | Viapo kwa waandikishaji wa wapiga kura, wasimamizi wa vituo na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi | 6-8 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa uchaguzi |
| 9. | Elimu kwa waandikishaji wa wapiga kura | 6-8 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 10. | Zoezi la uandikishaji wa wapiga kura | 11-20 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |

| Na. | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 11. | Kubandikwa kwa Orodha ya Wapiga Kura | 21 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 12. | Ukaguzi wa Orodha ya Wapiga Kura | 21-27 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 13. | Pingamizi kuhusu uandikishaji wa wapiga kura | 21-27 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 14. | Uamuzi kuhusu pingamizi | 27-28 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 15. | Marekebisho ya Orodha ya Wapiga Kura | 27-28 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |
| 16. | Kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa pingamizi | 28-29 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 17. | Uamuzi wa rufaa | 28-31 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 18. | Kukoma uongozi kwa viongozi waliopo madarakani | 25 Oktoba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 19. | Kuchukua fomu za kugombea | 01 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 20. | Kurejesha fomu za kugombea | 01-07 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 21 | Uteuzi wa Kamati ya Rufani | 01 Novemba, 2024 | Katibu Tawala wa Mkoa |
| 22. | Semina kwa kamati ya Rufani | 04 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 23. | Uteuzi wa wagombea | 8 Novemba, 2024 | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi |
| 24. | Uwasilishaji wa pingamizi kuhusu uteuzi | 8-9 Novemba, 2024 | Mwombaji/Mgombea/ |
| 25. | Uamuzi wa pingamizi kuhusu uteuzi | 8-10 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi Msaidizi |

| Na. | TUKIO | TAREHE | MHUSIKA |
|---|---|---|---|
| 26. | Kukata rufaa dhidi ya uamuzi kuhusu pingamizi la uteuzi | 10-13 Novemba, 2024 | Mwombaji/Mgombea/ Msimamizi wa Uchaguzi |
| 27. | Uamuzi wa kamati ya rufaa | 10-13 Novemba, 2024 | Kamati ya Rufani |
| 28. | Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kutoka katika Vyama vya Siasa | 14 Novemba, 2024 | Vyama vya Siasa/ Msimamizi wa Uchaguzi |
| 29. | Uwasilishaji wa ratiba za mikutano ya kampeni kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya | 17 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 30. | Kuanza kwa kampeni | 20-26 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |
| 31. | Siku ya Uchaguzi | 27 Novemba, 2024 | Msimamizi wa Uchaguzi |

KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI, TANZANIA